JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU SIKU YA HOMA YA INI DUNIANI TAREHE 28 JULAI, 2022.

**Dar Es Salaam, Tarehe 28 Julai, 2022.**

**Ndugu Wananchi,** tarehe 28 Julai ya kila mwaka, ni siku maadhimisho ya Homa ya Ini Duniani (World Hepatitis Day). Lengo kuu la maadhimisho haya ni kuielimisha na kuikumbusha jamii katika kutambua athari za ugonjwa wa Homa ya Ini, unavyoambukizwa, na namna ya kujikinga na ugonjwa huu.

Katika kuadhimisha siku hii, kila mwaka Shirika la Afya Duniani hutoa kauli mbiu yenye ujumbe maalum, unaolenga kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu madhara yanayotokana na ugonjwa huu. Kauli mbiu ya maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini Duniani kwa mwaka 2022 ni: **Kusogeza huduma za Homa ya Ini jirani na Jamii ("Bringing Hepatitis care closer to Communities").** Kauli mbiu hii inatulazimu kusogeza huduma kwa Jamii ili kudhibiti ugonjwa huu nchini na hatimaye kuweza kuutokomeza kabisa ifikapo mwaka 2030.

Homa ya Ini husababishwa na virusi ambavyo vipo katika makundi matano, yaani A, B, C, D na E.  Aina ya virusi vya A na E huambukizwa kwa njia ya kunywa maji na chakula kisichokuwa salama kwa kuchafuliwa na kinyesi chenye maambukizi ya virusi hivyo **("Faecal-oral Transmission")** ambazo dalili zinafanana kwa kiasi kikubwa na uambukizwaji wa magonjwa ya kuhara. Virusi aina ya B, C na D huambukizwa kwa njia sawa na za magonjwa ya ngono na VVU/UKIMWI kama kuongezewa damu yenye virusi vya ugonjwa

huo, kujamiiana, utumiaji usio salama wa sindano na kujichoma na vitu vyenye ncha kali, majimaji ya mgonjwa kumpata mtu mwingine kama ana kidonda, na pia mama anaweza kumwambukiza mtoto wake wakati wa kujifungua.Aina ya homa ya Ini inayosababishwa na virusi vya kundi B yaani Hepatitis B (HBV), ndiyo inayoongoza kwa maambukizi nchini..

Takwimu za Shirika la Afya Duniani kupitia taarifa ya Homa ya Ini ya mwaka 2021 zinaonesha kuwa, mwaka 2019, watu milioni 296 duniani, walikuwa wanaishi na Homa sugu ya Ini aina ya B ambapo zaidi ya nusu (66%) ya maambukizi hayo yalikuwa yanatoka katika Bara la Afrika. Aidha, watu wapatao milioni 58 walikua wanaishi na maambukizi ya Homa sugu ya Ini aina ya C. Wakati huo huo kulikuwa na vifo 820,00 duniani kutokana na Homa ya Ini aina B.

Kwa Tanzania, takwimu kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS) zinaonesha kuwa maambukizi ya Homa ya Ini aina ya B miongoni mwa wachangiaji damu kwa miaka mitatu ni kama ifuatavyo mwaka 2018 (**4.4%),** mwaka 2019 **(5.9),** mwaka 2020 **(6.1%)** na mwaka 2021 (**5.3%)**. Aidha, kwa kipindi hicho maambukizi ya Homa ya Ini aina C yameendelea kuwa ni ya **2.3%**.

Ugonjwa wa Ini aina ya A na E unaweza kuzuilika kwa kuboresha usafi wa mazingira, utayarishaji wa vyakula katika hali ya usafi na matumizi ya maji safi na salama. Ugonjwa wa Homa ya Ini aina ya B, C na D inazuilika kwa kutekeleza afua zote za kuzuia virus vya VVU/UKIMWI.

Kwa virus aina ya B ipo chanjo ambayo hutolewa kwa utaratibu wa kawaida wa utoaji wa chanjo kwa watoto wachanga. Chanjo hii ilianza kutolewa kwa watoto nchini waliozaliwa kuanzia mwaka 2002 (Pentavalent). Kwa kipindi cha mwaka 2021 utoaji wa chanjo ulifikia kiwango cha asilimia 98 ya watoto wote chini ya

miaka mitano walipata chanjo ya Pentavalent. Hakuna chanjo dhidi ya Homa ya Ini C, D na E.

Chanjo ya watu wazima hutolewa kwa watu walio kwenye makundi hatarishi. Makundi hatarishi kwenye maambukizi ya Homa ya Ini aina B na C ni Watumishi wa afya, Wanaume wanaofanya ngono na Wanaume wenzao, Watu wanaojidunga madawa ya kulevya, Watu wenye wapenzi wengi, watu wenye magonjwa sugu ya Ini, figo, kisukari na wenye upungufu wa kinga mwilini.

Matibabu ya Homa ya Ini hufanyika kulingana na aina ya maambukizi. Kwa wagonjwa waliopata virusi aina ya A na E, tiba yake mara nyingi hutolewa kutokana na dalili zinazoambatana na ugonjwa huu. Kwa wagonjwa waliogundulika kuwa na Homa ya Ini B matibabu hutegemea hatua ugonjwa aliyofikia, na wakati mwingine mgonjwa hulazimika kupewa dawa za kupunguza makali ya virusi vya ugonjwa huo kwa kipindi chote cha uhai wake. Aidha, kwa upande wa Homa ya Ini aina ya C tiba ipo na inachukua muda wa miezi mitatu hadi sita kukamilisha matibabu.

Hatua zinazofanyika na Wizara katika kudhibiti Homa ya Ini pamoja na;

1. Kusimamia Mpango Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti na Kutomeza Ugonjwa wa Homa ya Ini nchini wa mwaka 2018-2023.
2. Wizara pia imekamilisha Muongozo wa matibabu ya Homa ya Ini ambao utatumika kutoa maelekezo ya tiba hiyo nchi nzima ili kumpunguzia mwananchi gharama ya kusafiri umbali mrefu kwenda kupata tiba hiyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.
3. Kuandaa vielelezo vinavyohusu ugonjwa wa Homa ya Ini (Viral Hepatitis), ili kuuelimisha umma juu ya ugonjwa huu na namna gani maambukizi yanaweza kuzuiwa
4. Kuendelea kutoa elimu ya ugonjwa wa Homa ya Ini kupitia vyombo vya habari

5. Utaratibu wa kuwapatia mama wajawazito kinga ya kuzuia maambukizi ya Homa ya Ini aina B kutoka kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto zipo katika hatua za mwisho
6. Kuendelea na mchakato wa kuunganisha huduma ya homa ya Ini na mpango wa taifa wa kudhibiti UKIMWI nchini, ili iwe rahisi kuwekea mikakati ya kudhibiti ugonjwa huu

Kwa kuhitimisha, Siku ya Homa ya Ini, Wizara inatoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari ikiwa ni pamoja na kupata chanjo dhidi ya ugonjwa huu. Aidha, niwasisitize wadau wote katika sekta binafsi na umma kuendelea kuona umuhimu na kutoa kipaumbele na kuweka katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Ini nchini na hatimaye kuweza kuutokomeza kabisa ifikapo mwaka 2030.

**Mhe.Ummy A. Mwalimu (MB)**
**WAZIRI WA AFYA**